**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**

*Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe*
*Baraza la Madiwani,*
*Halmashauri ya Manispaa ya **I**lemela**.***
***MWANZA***

***YAH: TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA ROBO YA KWANZA (JULAI – SEPTEMBA) TAREHE 26/10/2017 MWAKA WA FEDHA 2017/2018***

## 1.0. UTANGULIZI

***Mhe. Mwenyekiti***, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa taarifa ya matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila robo ya mwaka.

***Hivyo taarifa hii itagusa maeneo yafuatayo:-***

i. *Taarifa ya Urasimishaji wa makazi holela katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri.*
ii. *Taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Mh Mkuu wa Mkoa ya juu utatuzi wa migogoro ya ardhi*
iii. *Taarifa ya ujio wa wageni kutoka nchi ya Korea Kusini kwa ajili ya kuja kuanza mradi wa usimamizi wa ardhi*
iv. *Taarifa ya ujio wa wageni kutoka shule ya Deby Grammer nchini Uingereza.*
v. *Taarifa ya Ugeni kutoka United Nations Capital Development Fund (UNCDF)*
vi. *Taarifa ya maendeleo ya mradi wa uendelezaji Miji na Majiji (TSCP)*
vii. *Taarifa ya Maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa ALAT*

## 2.0. UFAFANUZI WA TAARIFA

### 2.1 Taarifa ya Urasimishaji wa makazi holela katika maeneo mbalimbali ya halmashauri.

Ili kudhibiti makazi yasiyo rasmi Halmashauri inaendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuboresha makazi kwa kufanya upimaji shirikishi ambapo katika zoezi la kurasimisha makazi, viwanja 28,815 vilitarajiwa kupimwa na kupatiwa Hati ifikapo Mwezi Juni 2017. Hadi sasa jumla ya viwanja 14,905 vimekwisha kupimwa na Hati milki 2,067 zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa kamishina

msaidizi wa kanda. Aidha, viwanja 13,910 viko kwenye hatua mbalimbali za upimaji na rasimu za hati 1640 zinaendelea kuandaliwa.
Pamoja na mafanikio hayo hapo juu, kumekuwepo na changamoto nyingi katika utekelezaji wa zoezi hili ambazo ni;

1. Mwitikio mdogo wa wananchi katika kuchangia gharama za upimaji na kuandaliwa Hati milki, Mathalani, kwa Mwezi Agosti wananchi 101 pekee ndiyo w walilipia gharama za Hati milki.
2. Wananchi kutokuwasilisha nyaraka muhimu za kukamilisha Hati milki kama Uthibitisho wa Uraia, picha n.k.
3. Migogoro iliyotokana na Wananchi kutokuwa tayari kuachia maeneo ya huduma za jamii, kama vile, barabara, masoko, maeneo ya wazi n.k. hivyo kuchelewesha ukamilishaji wa Ramani za Upimaji na Umilikishaji.
4. Wananchi kuvamia maeneo yaliyotengwa na kupimwa kwa shughuli za huduma za jamii kama vile Zahanati, maeneo ya wazi na kutokuwa tayari kuchangia upatikanaji wa maeneo mbadala ya huduma hizo muhimu.

Pamoja na changamoto zilizojitokeza, Halmashauri imekuwa ikizikabili kwa njia mbalimbali ambazo ni pamoja na;-

- Kufanya mikutano ya kuhimiza wananchi kulipia gharama za Upimaji na Umilikishaji katika Kata zinazohusika. Waheshimiwa Madiwani na Mhe Mbunge wa Jimbo la Ilemela walishiriki kikamilifu katika mikutano hiyo. Aidha, matangazo kwa kutumia gari la matangazo, Pembe kwenye Mitaa husika na vyombo vya habari vya Radio na Televisheni yamefanyika.
- Wataalamu kuwafuata wananchi na kuwahudumia kwenye Ofisi za Watendaji wa Kata ambapo malipo yote yalifanyika kwa kutumia wakala wa Benki ya NMB. Kata zilizofikiwa ni Nyasaka, eneo la Nundu Kata ya Mecco, eneo la Ibanda Juu Kata ya Kirumba. Hii ilitia hamasa na wananchi wengi walijitokeza kuja kulipia.

- Watendaji wa Kata na Mitaa walitumiwa orodha ya wananchi ambao hawajaleta viambatanisho vya Hati milki kwa ufuatiliaji, pia taarifa kwa njia ya simu kwa wahusika zilitolewa.

- Vikao vya uelimishaji kwa wananchi vikihusisha viongozi wa Mitaa na Kamati za Urasimishaji ili kuachia maeneo hayo ya huduma muhimu vilifanyika.

Ili kuweza kufikia lengo lililokusudiwa, tunaendelea kuwahimiza wananchi wote wanaohusika na zoezi hili kuchangia kwa wakati kwani zoezi litakoma rasmi ifikapo 30/10/2017 na wale wote ambao hawatalipia watahitajika kufuata mpango wa matumizi ulioandaliwa kupitia Mpango kabambe wa Jiji la Mwanza.

### 2.2 Taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Mh Mkuu wa Mkoa juu ya utatuzi wa migogoro ya ardhi

Mnamo tarehe 13/09/2017 Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mwanza alifanya Mkutano na wananchi kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero za ardhi katika viwanja vya Makao Makuu ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela. Jumla ya wananchi 218 walijiorodhesha na wananchi 139 waliwasilisha, kusikilizwa na kutatuliwa kero zao. Wananchi wapatao 79 hawakujitokeza kuwasilisha malalamiko yao walipoitwa licha ya kujiorodhesha.

Mhe. Mkuu wa Mkoa alisikiliza kero za wananchi na kutoa maagizo kwa Mkurugenzi wa Manispaa ili kutekeleza kero hizo. Maagizo hayo ni kama ifuatavyo;-

(a) Kuwapatia viwanja wananchi ambao mashamba yao ya asili yalipimwa na kugawiwa wananchi wengine,
(b) Kulipa fidia wananchi ambao maeneo yao yalitwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa Taasisi za umma na kwenye miradi ya upimaji wa viwanja,
(c) Kupima maeneo ya wananchi kwa kufanya mgawanyo au kuyabadilisha matumizi.

Wataalamu wa Idara ya Mipango Miji walipokea maelekezo na kuyafanyia kazi kwa kutembelea na kufanya ukaguzi wa maeneo yaliyolalamikiwa wakishirikiana na Walalamikaji, Viongozi wa Mitaa na Kata husika.

#### 2.2.1 Utekelezaji wa maagizo

**(A) Madai ya viwanja.**

Wananchi wapatao 86 walilalamikia kutokupewa viwanja vilivyopimwa katika mashamba wanayodai kuyamiliki kiasili baada ya kupimwa na kumilikishwa kwa watu wengine.

**Agizo Na. 01**

Mh. Mkuu wa Mkoa aliagiza wananchi wenye madai ya aina hii wamilikishwe baadhi ya viwanja ambavyo vilikwisha milikishwa kwa wananchi wengine na wao kutopewa viwanja kwenye mashamba yao ya asili baada ya ufutaji wa milki za awali kufanyika.

**Utekelezaji**

Ukaguzi wa viwanja katika maeneo yaliyolalamikiwa ulifanyika na kubaini baadhi ya viwanja vilishaendelezwa na vingine havijaendelezwa. Kwa viwanja ambavyo havijaendelezwa taratibu za kufuta milki hizo kwa mujibu kanuni za mwaka 2001 zimeanza na tayari wamiliki hao ambao hawajaendeleza viwanja hivyo wametumiwa barua za onyo.

Baada ya siku 30 Mmilki aliyetumiwa barua anatakiwa kuwasilisha utetezi wake juu ya masharti ya uendelezaji yaliyokiukwa, wale watakaoshindwa kutekeleza watapewa Ilani ya siku 90 ya kusudio la kufuta miliki zao kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999.

Walalamikaji wa madai ya viwanja wameandikiwa barua za kuwajulisha hatua zilizochukuliwa na Mamlaka.

**(B) Madai ya fidia**

Wananchi wapatao 23 walilalamikia kutolipwa fidia ya maeneo yao yaliyotwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umma zikiwemo Shule, Zahanati,Masoko pamoja na maeneo ya miradi ya upimaji wa viwanja 3500 ya Kiseke,Buswelu na Nyamhongolo.

**Agizo Na. 02**

Ifikapo tarehe 01/ 01/2018 Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela awe amelipa wananchi wote wanaodai fidia. Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza ifikapo tarehe 15/09/2017 awe amewasilisha taarifa zote za uthamini zilizofanyika kabla ya kuanzishwa kwa Manispaa ya Ilemela ili kuwezesha Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kutekeleza agizo hili.

**Utekelezaji**

Tarehe 29/09/2017 tulipokea taarifa za uthamini kutoka Jiji la Mwanza kwa barua yenye Kumb. Na. MCC/L/72123/37 ya tarehe 18/09/2017. Tunaendelea kufanya uchambuzi kubaini madeni halali ya fidia yanayopaswa kulipwa. Wananchi wanaodai fidia na ambao taarifa zao zimeonekana ni sahihi wameandikiwa barua za kuwajulisha. Uchambuzi wa taarifa hiyo ya uthamini bado unaendelea. Aidha, taarifa za Uthamini zilizowasilishwa hazijakamilika kuwezesha kujua mchanganuo wa madai ya msingi ya walalamikaji.

Aidha, changamoto kubwa inayokablili Halmashauri katika kutekeleza ni madai makubwa ya fidia takribani Tsh. 5,000,000,000/= kwenye maeneo mbalimbali yaliyotwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umma yakiwemo maeneo ya Shule, Zahanati, Barabara, Masoko, Maeneo ya Wazi na mradi wa viwanja 3500 uliohusisha maeneo ya Kiseke, Nyamhongolo na Buswelu.

**(C) Malalamiko ya upimaji**

Wananchi wapatao 30 walilalamikia maeneo yao kutopimwa na wengine kuwa na mwingiliano wa mipaka ya viwanja.

**Agizo Na. 03**

Wananchi wapimiwe maeneo yao na mipaka ya viwanja yenye mwingiliano irekebishwe.

**Utekelezaji**

Wapima ardhi walitembelea maeneo yaliyolalamikiwa na kubaini kuwa maeneo mengine hayana sifa za kufanyiwa upimaji kwani yapo kwenye maeneo hatarishi na mengine kuwa katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya miundombinu ya jamii kama hifadhi ya barabara na maeneo ya wazi. Baadhi ya maeneo hayo ni eneo lililopo Iloganzala karibu na Kiwanda cha Coral Paints linalolalamikiwa na ndugu Mkoka Gunza na Wenzake kuwa katika hifadhi ya Mto.

Aidha, malalamiko yalitolewa kwenye maeneo yanayotekeleza zoezi la Urasimishaji wa Makazi, utatuzi wake ulifanyika kwa kuhusisha Kamati za Upimaji za Mitaa husika na Viongozi wa Mitaa.

**2.3 Taarifa ya ujio wa wageni kutoka Nchi ya Korea Kusini**

**Mhe: Mwenyekiti**, mnamo tarehe 26/09/2017 Halmashauri ilipokea wageni kutoka nchi ya Korea Kusini. Wageni hawa ni mwendelezo wa programu na makubaliano ambayo Halmashauri iliingia na wawekezaji kutoka nchi ya Korea Kusini. Hivyo kutokana na ujio huo, zifuatazo ni shughuli zitakazotekelezwa

(a) Kuanzisha kanzi data kwa ajili ya kuwa na taarifa zote za masuala ya ardhi kidigitali ambapo itatumika katika ukusanyaji wa mapatao ya Serikali, ulinzi na usalama, kupunguza migogoro ya ardhi na upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa muda.

(b) Kuanzisha mfumo wa kusimamia na kutoa huduma za ardhi

(c) Kuwajengea uwezo wataalamu wa Halmashauri ya Manispaa ndani na nje ya nchi

(d) Kufanya upangaji na upimaji wa ardhi kwa kutumia teknolojia ya kisasa (ndege ndogo – Drones/UAV)
(e) Wizara ya ardhi, miundombinu na usafirishaji ya nchi ya Korea kusini kwa kushirikiana na shirika la LX zimetengwa jumla ya Dola za Kimalekani 500,000 kwa ajili ya kazi hii.

### 2.4 Taarifa ya ujio wa wageni kutoka Deby Grammar School - Uingereza

**Mhe: mwenyekiti,** Halmashauri yetu manamo tarehe 19/10/2017 ilipata bahati ya kutembelewa na wageni watatu kutoka **Derby Grammar School ya Uingereza.** Shule hii ni rafiki na Shule ya Msingi Gedeli B (Ibeshi) iliyopo Wilaya ya Ilemela Mwanza. Wageni hawa walifika katika halmashauri yetu na wakaongea na Menejimenti ya Manispaa.

Katika miaka mitatu iliyopita shule hiyo imetusaidia kujenga vyoo, madarasa manne, vifaa vya kujifunzia na kufundishia vifaa vya michezo na wamesawazisha uwanja na kujenga mtalo wa kuzuia maji. Kwa mwaka ujao wanatarajia kujenga bweni la wanafunzi walemavu na uzio. Programu hii itakuwa ya miaka kumi kuanzia mwaka 2013 hadi 2022

### 2.5 Taarifa ya ujio wa wageni kutoka Mfuko wa Mtaji wa Kimataifa (UNCDF)

Mnamo tarehe 11/10/2017, Halamshauri ya Manispaa ya Ilemela ilipata wageni kutoka United Nations Capital Development Fund. Wageni hawa walifika kwa ajili ya kuja kujadiliana na Menejimenti juu ya miradi itakayofaa kufadhiliwa kupitia Hisa za Halmashauri ya Manispaa (Municipal Bonds).

Pia ujio huo ulifika kwa ajili ya kutekeleza maamuzi ya hivi karibuni kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na Mfuko wa Mitaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF), Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela iliarifiwa na Katibu Mkuu OR-TAMISEMI kwa barua yenye kumb. Na PPP/A/01/01 kuwa imeingizwa rasmi na itanufaika kupitia mpango huu. Tarehe 04/10/2017, UNCDF walionesha nia na kuiandikia barua Halmashauri yetu kuhusu kujengewa uwezo ili kuweza kupata mitaji na kutekeleza mirandi mbalimbali ya maendeleo kupitia mikopo hii ya Manispaa.

Mnamo tarehe 11/10/2017 Ujumbe kutoka OR-TAMISEMI na UNCDF uliwasili katika ofisi za Manispaa ya Ilemela na kufanya mazungumzo ya pamoja na Mhe. Meya, Katibu wa Mbunge, Timu ya Menejimenti ya Halmashauri (CMT) na Timu ya Uwekezaji ya Halmashauri. Majadiliano hayo yalikuwa juu ya

Mipango ya Uwekezaji wa mitaji, aina ya miradi ya maendeleo yenye tija kibiashara na utayari wa Halmashari katika utekelezaji wa mipango hiyo. Katika mazungumzo hayo, pamoja na mambo mengine, miradi ya maendeleo yenye tija kibiashara ilijadiliwa. Ifuatayo ni orodha ya miradi iliyopendekezwa kwa ajili ya utekelezaji.

i. Ujenzi wa soko la Kiloleli
ii. Ujenzi wa Nyumba za kupangisha -Kirumba (Kirumba Real Estate)
iii. Ujenzi wa Kituo Maalumu cha Vipimo vya Magonjwa (Specialized Diagnosis Centre)
iv. Ujenzi wa Uwanja wa Michezo Ilemela

Aidha, wataalam kutoka UNCDF na OR-TAMISEMI walishauri kwamba, ili kuanza kutekeleza mpango huu taarifa muhimu zifuatazo lazima ziandaliwe na kuwasilisha OR-TAMISEMI ndani ya kipindi cha mwezi mmoja kutoka siku hiyo ya kikao.

i. Rasimu za maandiko ya miradi (Project Concept Notes)
ii. Mpango wa Kibiashara (Business Plan)
iii. Michoro (Architectural drawings)
iv. Mchangnuao wa gharama za Viwango (BOQ)

2.6 **Taarifa ya Maendeleo ya Mradi wa TSCP**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, ili kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa 2015, Halmashauri ya Manispaa katika mwaka wa Fedha 2017/2018, ilipanga kujenga barabara ya lami kutoka Buswelu – Kiseke – sabasaba yenye urefu wa kilomita 10. Ninayofuraha kubwa kulijulisha Baraza hili kuwa, kazi ya ujenzi itaanza mwezi Januari 2018 kwani mpaka sasa zabuni imefunguliwa na tathmini iko hatua za mwisho. Barabara hii inafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Tanzania, Benki ya Dunia kupitia mradi wa uendelezaji miji na Majiji (TSCP) kwa kushirikiana na Halmshauri ya Manispaa ya Ilemela.

Aidha, Jumla ya fedha kiasi cha **Tshs 636,626,000** kinatakiwa kulipwa Wananchi ikiwa ni mchango wa Halmashauri kwenye mradi huu kwa mujibu wa makubaliano ifikapo mwezi Disemba, 2017

Napenda kutoa wito kwa waheshimiwa Madiwani na wananchi kwa ujumla kushirikana wakati wa utekelezaji wa mradi huu pindi utakapoanza kutekelezwa ili kusiwe na mkwamo utakaotokana na malalamiko yasiyokuwa ya msingi.

## 2.7 Taarifa ya Maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kufungua mkutano Mkuu wa 33 wa ALAT Taifa

Mnamo tarehe 03/10/2017, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt John Pombe Joseph Magufuli alitoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika hotuba yake ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa33 wa ALAT Taifa 03/10/2017 Uliofanyika katika ukumbi wa Mwalimu Julius Nyenyere – Dar Es Salaam. Baadhi ya mambo muhimu aliyoelekeza Mheshimiwa Rais ni**;**

(i) Mamlaka za Serikali za Mitaa kubuni mikakati ya kushughulikia matatizo ya upungufu wa vyumba vya madarasa, maabara, vyoo na nyumba za walimu;

(ii) Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kuwa zinawahimiza wananchi wote kuwapeleka watoto wao shule ili waweze kunufaika na mpago maalumu wa Serikali wa elimu bila malipo;

(iii) Pamoja na Serikali kuwa na mpango maalumu wa upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya, Mheshimiwa Rais aliziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinaweka mpango mkakati wa kukabiliana na upungufu wa miundombinu katika Hosptitali, vituo vya afya , zahanati na nyumba za watumishi;

(iv) Waheshimiwa madiwani wawahamasishe Wananchi ili kujiunga na mifuko ya bima ya Afya ili kuweza kupata matibabu bila kikwazo;

(v) Kusimamia vema matumizi ya dawa ikiwa ni pamoja na kuanzisha mfuko wa dawa (Drug Revolving Fund) kwa kila Halmashauri ili kuhakikisha upatikanaji wa fedha za dawa endelevu;

(vi) Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Hivyo kubuni mifumo madhubuti ya ukusanyaji wa mapato, hususani kwa njia ya kielektroniki na kuendelea kubuni vyanzo endelevu vya mapato;

(vii) Kusimamia vizuri matumizi ya fedha zinazokusanywa na zinazoletwa na Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo ili kuendana na thamani ya fedha na kuchukua hatua za kinidhamu kwa wale wote watakaojihusisha na ubadhilifu;

(viii) Wajumbe waache kutoa zabuni kwa makampuni yao au washirika wao na wazabuni wasio na uwezo;

(ix) Kudhibiti migogoro na kuacha makundi miongoni mwa Wahe. Madiwani na watendaji na viongozi ndani ya Wilaya kwani hupunguza kasi ya kuwapelekea wananchi maendeleo;

(x) Kushughulikia kero za wananchi hususani wenye kipato cha chini kwa kupunguza utitiri wa kodi na kuwapatia maeneo ya kufanyia biashara wafanyabiashara wadogowadogo; na

(xi) Kuwahimiza wananchi kudumisha Amani na umoja, kulipa kodi na kuchapa kazi kwa bidii.

Naomba kuwasilisha**.**

John Paul Wanga
Mkurugenzi wa Manispaa
**ILEMELA**